

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**638**


**VIELELEZO NA TEKNOLOJIA**

**Muda: Saa 3**

**Jumatatu, 14 Mei 2018 asubuhi**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **manne (4)** kutoka katika sehemu B.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha **mtihani**.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



## SEHEMU A (alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Ainisha changamoto nne za kutumia luninga kama kielelezo na teknolojia ya kufundishia na kujifunzia.
2. Ainisha sifa nne za vielelezo na teknolojia bora za kufundishia na kujifunzia.
3. Kwa hoja nne, tofautisha kati ya vielelezo na teknolojia asilia na vielelezo na teknolojia kisasa.
4. (a) Eleza kwa kifupi maana ya ubao wa kufundishia na kujifunzia.  
(b) Ainisha changamoto tatu ambazo waalimu wanakutana nazo katika kutumia ubao wa chaki kwa ajili ya kufundisha na kujifunzia.
5. Bainisha hatua nne utakazozingatia katika kutengeneza sinia la namba.
6. Eleza kwa kifupi chimbuko la vielelezo na teknolojia asilia. Toa hoja Nne.
7. Kwa kutumia hoja nne eleza jinsi simu inavyoweza kutumika katika ujifunzaji na ufundishaji.
8. Eleza kwa kifupi mapungufu manne ya vielelezo na teknolojia ya kukodi.
9. Kwa kifupi eleza ni kwa nini njia ya kutengeneza vielelezo na teknolojia haitumiwi na walimu mara kwa mara.
10. Panga vielelezo vifuatavyo katika makundi ya vielelezo na teknolojia maono, masikizi na masikizi maono.
  - (a) Maandishi
  - (b) Nyimbo
  - (c) Grafu
  - (d) Radio Kaseti
  - (e) Luninga
  - (f) Michoro
  - (g) Video
  - (h) Ngoma

## SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **manne (4)** kutoka katika sehemu hii.

11. Kwa kutumia mifano, chambua faida tano za ubao wa chaki katika kumsaidia mwalimu na mwanafunzi katika ujifunzaji na ufundishaji.
12. Eleza umuhimu wa vielelezo na teknolojia mpitisho.
13. Kwanini ni muhimu kwa mwalimu kutunza vielelezo na teknolojia? Toa hoja tano.
14. Kwanini vielelezo na teknolojia asilia havitumiki sana katika kufundishia. Toa hoja tano.
15. Eleza madhara matano yatakayojitokeza endapo mwalimu atatumia vielelezo na teknolojia visivyo na ubora katika ufundishaji na ujifunzaji.
16. Fafanua manufaa matano ya mwalimu kuzingatia msingi wa uchoraji wa michoro na vipimo katika uandaji wa vielelezo na teknolojia mbalimbali vya ufundishaji na ujifunzaji.